

# Haki Zako ukiwa katika Kituo cha Polisi



Watu wengi hawaelewi

utaratibu unaofuatwa katika kituo cha polisi.



Polisi wanapotaka kukuuliza maswali,

ni vyema uwajulishe iwapo unahitaji usaidizi

na ikiwa huelewi.




Polisi wanatambua kuwa





wanaotatizika na mawasiliano wanahitaji

muda zaidi kusoma na kujibu

maswali.

## Yaliyomo

	<p>Kukamatwa na kupelekwa kwenye kizuizi cha polisi</p>	<p>Ukurasa wa 4</p>
	<p>Kujibu maswali unayoulizwa na polisi</p>	<p>Ukurasa wa 5 - 6</p>
	<p>Kuomba Usaidizi wa Mtu Mzima</p>	<p>Ukurasa wa 7</p>
	<p>Kumwarifu wakili umepelekwa kwenye kituo cha polisi</p>	<p>Ukurasa wa 8</p>
	<p>Kumwarifu mtu mwingine umepelekwa kwenye kituo cha polisi</p>	<p>Ukurasa wa 9</p>
	<p>Ikiwa una miaka 16 au hujafikisha umri huu, au ikiwa una miaka 16 au 17 na uko chini ya usimamizi.</p>	<p>Ukurasa wa 10 - 11</p>

	<p>Je, hatua gani itachukuliwa ukishtakiwa au ukipelekwa kituoni kufuatia agizo la kukamatwa?</p>	<p>Ukurasa wa 12 - 13</p>
	<p>Je, unaweza kukamatwa kwenye kituo cha polisi kwa muda gani?</p>	<p>Ukurasa wa 14</p>
	<p>Kuona daktari au muuguzi</p>	<p>Ukurasa wa 15</p>
	<p>Kuwasilisha malalamiko</p>	<p>Ukurasa wa 16</p>



## Kukamatwa na kupelekwa kwenye kizuizi cha polisi

Polisi watakueleza sababu ya kukamatwa.



Polisi watakuuliza ikiwa unaelewa.

Iwapo huelewi kitu fulani, unapaswa kusema “la”.

Sema “ndiyo” ikiwa unaelewa.

## Kujibu maswali unayoulizwa na polisi



Una haki ya kukaa kimya.

Unaweza **kutojibu** maswali unayoulizwa na polisi. **HATA HIVYO**, unapaswa kuwaeleza–

**jina lako**



**unakoishi**



**tarehe yako ya kuzaliwa**



**ulikojaliwa na  
utaifa wako**

**Ikiwa hujui baadhi ya maelezo haya  
unapaswa kuwaambia polisi.**

**Sio kosa usipojibu maswali mengine.**

Polisi watakueleza kuwa wataandika yote  
utakayosema.

Ukiamua kujibu maswali, chochote  
utakachosema kinaweza kutumika kama  
ushahidi kesi yako ikiyelekwa mahakamani.





## **Kuomba Usaidizi wa Mtu Mzima**



Ikiwa unahitaji usaidizi, waambie polisi **“mpigie simu Mtu Mzima Atakayenisaidia”**.

Mtu Mzima Atakayekusaidia ni yule anakufafanulia kile polisi wanachosema. Huduma hii hailipishwi.



Mtu Mzima Atakayekusaidia atakueleza kuhusu haki zako na kinachoendelea.

Atakufafanulia maswali unayoulizwa na polisi ikiwa huelewi.

Kando na kukufafanulia kile polisi wanachosema, atakueleza wanachofanya.



Mtu Mzima Atakayekusaidia hawezi kukupa ushauri.

Polisi watamwita Mtu Mzima Atakayekusaidia ikiwa wanaamini kuwa unahitaji usaidizi, hata usipoomba.

**Ni muhimu kusema ikiwa huelewi.**

## **Kumwarifu wakili umepelekwa kwenye kituo cha polisi**



Una haki ya kuzungumza na **wakili** faraghani wakati wowote kabla ya kuulizwa maswali. Huduma hii hailipishwi.

**Wakili ni mtu anayelinda haki zako na kukutetea.**

Mtu Mzima Atakayekusaidia hapaswi kuwepo unapozungumza na wakili wako.

Ikiwa ungependa kuzungumza na wakili, unapaswa kusema “ndiyo” polisi watakapokuuliza.



Iwapo una wakili, unapaswa kuwapa polisi jina lake. Polisi watampigia simu. Huduma hii hailipishwi.

Ikiwa huna wakili unahitaji kuwaambia polisi ili wakutafutie.

Polisi watawasiliana na wakili wako haraka iwezekanavyo. Huduma hii hailipishwi.



Wakili anaruhusiwa kuwepo unapohojiwa na polisi. Huduma hii hailipishwi.

Unaweza kuzungumza na wakili wako kwa simu au anaweza kuja kituoni kukuona. Uamuzi ni wake.

Utaulizwa kwa mara ya pili ikiwa ungependa wakili awepo unapohojiwa hata ikiwa tayari umezungumza naye kwa simu.



## **Kumwarifu mtu mwingine umepeleka kwenye kituo cha polisi**



Una haki ya mtu mwingine kujulishwa kuwa upo kituoni.

Polisi watakuuliza mtu ambaye ungependa apigiwe simu.



Huyu anaweza kuwa mwanafamilia, mwenzako, mlezi, rafiki yako au mtu mwingine mnayefahamiana.

Huenda usiruhusiwe kuzungumza na mtu huyu.

**Ikiwa una miaka 16, au ikiwa una umri wa miaka 16 au 17 na uko chini ya usimamizi:**



Sharti polisi wajulishe mzazi au mlezi wako kwamba uko kituoni.



Una haki ya kutembelewa na mzazi au mlezi kwenye kituo cha polisi.

Walio chini ya miaka 18 pekee ndio wanaruhusiwa kutembelewa.



Wakili wako sharti awepo polisi wanapokuhoji, isipokuwa katika hali **zisizo za kawaida**.



Kwa mfano, iwapo polisi wanaamini kuwa una taarifa muhimu itakayowawezesha kumwokoza mtu, huenda ukaulizwa maswali kabla ya wakili wako kufika.

Ikiwa una umri wa miaka 16 au 17 na uko chini ya usimamizi au uangalizi wa kisheria kwa muda, HURUHUSIWI kukataa wakili.

Hata katika hali zisizo za kawaida, una haki ya kukaa kimya.



**Je, hatua gani itachukuliwa ukishtakiwa au ukipelekwa kituoni kufuatia agizo la kukamatwa?**



**Ukishtakiwa, unaweza kuruhusiwa kuondoka au unaweza kusalia korokoroni kisha ufike mahakamani siku inayofuata.**



Ukishtakiwa, polisi watanasa yafuatayo:

- **alama zako za vidole**



- **sampuli ya DNA** (watatia mrija mdogo wenye pamba mdomoni mwako)



- **picha yako**



Iwapo umefikishwa kituoni kufuatia **agizo la kukamatwa**, utalala kwenye seli kisha ufikishwe mahakamani siku inayofuata.



**Je, unaweza kukamatwa kwenye kituo cha polisi kwa muda gani?**



Polisi wanaweza kukukamata kwa **hadi saa 12** bila kukushtaki kwa kosa la uhalifu.




Polisi watakupa chakula wakati wa mlo ukikamatwa kwa zaidi ya saa 4.

Ikiwa vipo vyakula vinavyokudhuru, wajulishe polisi haraka iwezekanavyo.

Ukiwa na kiu, waombe polisi maji.



Polisi wanaweza kukukamata **hadi saa 24 ikiidhinishwa na Inspekta wa Polisi** (au Inspekta Mkuu ikiwa hujafikisha miaka 18).



Una haki ya kutoa maoni yako kuhusu uamuzi huu, au unaweza kumpa wakili nafasi azungumze na polisi kwa niaba yako.



## Kuona daktari au muuguzi

Una haki ya kumwona **daktari** au **muuguzi** ikiwa wewe ni mgonjwa au umejeruhiwa.

Wajulishe polisi ikiwa unaamini unahitaji kumwona daktari au muuguzi.

Ni muhimu uwaeleze polisi ikiwa una matatizo ya kiafya au unatumia dawa.



Pia ni muhimu kuwajulisha Polisi ikiwa una uraibu wowote wa dawa za kulevya au pombe, au ikiwa unawaza kujidhuru.



**Hii itawasaidia Polisi kukushughulikia ukiwa kwenye seli.**



## Kuwasilisha malalamiko



Una haki ya **kuwasilisha malalamishi** kuhusu jinsi ulivyotendewa na polisi.

Kuwasilisha malalamishi dhidi ya Polisi wa Skoti hakutaathiri kesi yako.

Unaweza kuwasilisha malalamiko ukiwa korokoroni.

Ikiwa ungependa kuwasilisha malalamishi ukiwa korokoroni, omba uzungumze na inspekta au afisa wa cheo cha juu.



Iwapo ungependa kuwasilisha malalamiko baada ya kuachiliwa, unaweza kwenda kituo chochote cha polisi.

Ikiwa umeumizwa au kujeruhiwa na afisa wa polisi wakati wa kukamatwa au ukiwa korokoroni, unapaswa kuwasilisha malalamiko kwa Idara ya Viwango vya Kitaalamu ya Polisi wa Skoti.

Ili kuwasilisha malalamiko, piga simu kwa 101 au nenda kwenye kituo cha polisi kilicho karibu nawe.

Unaweza pia kumwomba mtu mwingine awasilishe malalamiko kwa niaba yako. Inaweza kuwa mzazi, rafiki, mwenzako au mtu unayemwamini.

Unahitaji kutoa idhini yako kwa kuandika.



Imetayarishwa kwa niaba ya

**SOLD Network**

na

**People First (Scotland)**


**77-79 Easter Road,**

**Edinburgh,**

**EH7 5PW**

**0131 478 7707**

Kampuni isiyo ya faida, nambari  
173180 na Shirika la Uhisani  
Lililosajiliwa Uskoti, Nambari SC  
026039



**People First  
(Scotland)**



**POLICE  
SCOTLAND**

Keeping people safe

---

**POILEAS ALBA**